**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA**

# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W) TAREHE 29/12/2021.

## AGENDA ZILIZOJADILIWA

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita
4. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao kilichopita
5. Taarifa ya mapato na matumizi kuishia Mwezi Novemba 2021
6. Taarifa ya Mapokezi ya fedha Tshs 390,000,000/= na kuwasilisha mgawanyo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharula (EMD) na ujenzi wa nyumba ya mtumishi (3/1) katika kituo cha afya Kirumi.
7. Mapendekezo ya mahaulisho (marekebisho ya Bajeti) ya Mwaka2021/2022
8. Taarifa ya zoezi la chanjo dhidi ya ugonjwa wa mapele ngozi kwa Mifugo
9. Mengineyo
10. Kufunga Kikao.

## WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Mhe. Peter W. Nyerere - Mwenyekiti H/W Butiama - Mwenyekiti
2. Ndg. Alphonce Mlewa - kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) – Katibu
3. Mhe. Bhoke Ngurube - Mjumbe
4. Mhe. Juma M. Sendi - Makamu M/kiti
5. Mhe. Willy B. Nyamtiga - Mjumbe
6. Mhe. Daudi C. Kisangure - Mjumbe
7. Mhe. Paul W. Meha - Mjumbe
8. Mhe. Magina M. Nyauko - Mjumbe
9. Mhe. Nyagheti J. Adam - Mjumbe

## WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

1. Mhe. Jumanne A. Sagini - Mjumbe – Kwa taarifa

**WAJUMBE (WATAALAM) WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Christian Makebe - Kaimu Afisa Utumishi (W)
2. Ndg. Demetria Leshabari - kaimu Mganga Mkuu (W)
3. Ndg. Chaina Masamaki - Afisa Manunuzi
4. Ndg. Leonard Lukawe - Mweka Hazina (W)
5. Ndg. G.Ulonginagani - Afisa Mipango Miji (W)
6. Ndg. Pendo Masalu - kaimu Afisa Elimu (S)
7. Ndg. Leopold costantine - Kaimu A/Maendeleo ya jamii (W)
8. Ndg. Edward Mturi - Afisa Mifugo/Uvuvi (W)
9. Ndg. Revocatus Lutunda - Afisa Kilimo (W)
10. Ndg. Clementina Mutakyamirwa - kny. Mratibu TASAF
11. Ndg. Julius Wambura - Afisa TEHAMA
12. Ndg. Sogone R. Wambura - Kaimu A/Uchaguzi
13. Ndg. Kedmon Chipanyanga - A/Maliasili Ardhi na Mazingira
14. Ndg. Wumbe E. Harun - Mhasibu Mapato
15. Ndg. Titus J Kamwaga - kaimu Afisa Elimu Msingi
16. Ndg. Karani Ruhumbika - Kaimu Afisa U/Mazingira
17. Ndg. Mtani N James - Mwandishi wa Mikutano
18. Ndg. Joseph Lyakurwa - Sheria
19. Ndg. Nyarara Majiwa - Afisa Utumishi

**KUMB NA KFUM/04/18/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:27 asubuhi. Aliwasisitiza wajumbe wote kushiriki kikamilifu katika kujadili agenda zilizowasilishwa ili kuleta maendeleo kwenye Halmashauri na Wilaya kwa ujumla.

**KUMB NA KFUM/04/19/2021/2022 KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA.**

Muhtasari wa kikao kilichopita uliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa. Ulifanyiwa marekebisho pamoja na masahihisho kisha uliwekewa saini kama kumbukumbu sahihi.

**KUMB NA KFUM/04/20/2021/2022 YATOKANAYO**

**1. SUALA LA UJENZI WA CHOO CHA MNADA WA KIABAKARI**

Wajumbe katika kikao hawakuridhishwa na majibu ya utekelezaji wa azimio hilo,hivyo kikao kiliazimia kwa mara nyingine kwamba, Afisa Mifugo, Mhandisi wa ujenzi pamoja wahe. Madiwani wa katahusika wakutane kwenye eneo la mradi ili kujiridhisha na hali ya ujenzi wa shimo linaloelezwa kuwa limefunikwa pasipo kujengewa.

**2. SUALA LA MENEJIMENTI KUKUTANA NA BW.GIMUNTA MMILIKI WA ENEO MAKUTANO(Zerozero) KWA AJILI YA MAZUNGUMZO JUU YA HALMASHAURI KUTAKA KUTWAA ENEO HILO.**

Kwa kuwa hadi tarehe ya kikao hicho suala hili lilikuwa halijatekelezeka, kamati ilisisitiza kwamba Menejimenti iendelee kufuatilia suala hilo kwa muhusika.

3. **SUALA LA MIRADI YA UJENZI WA VYOO VYA MAGUNGA PAMOJA NA SIRORISIMBA.**

Katika kikao hicho, wajumbe hawakuridhishwa na majibu ya utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kiasi cha fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo hivyo. Hivyo basi kamati iliazimia kwamba miradi ya vyoo hivyo itengewe na kupelekewa fedha kiasi cha Tsh. Milioni sita kwa kila choo**.**

4. **SUALA LA MWENYEKITI WA HALMASHAURI KUKABIDHIWA TAARIFA YA MAPATO KATIKA SIKU ZAKE MBILI ANAPOKUJA OFISINI.**

Kikao kiliazimia kwmba Menejimenti itoe taarifa hiyo kwa Mwenyekiti anapokuja Ofisini siku mbili za kila wiki.

5. **SUALA LA UNUNUZI WA VIFAA TIBA KATIKA ZAHANATI YA BUTUGURI KUPITIA FEDHA ZA MFADHILI ZILIZOLETWA.**

Kutokana na fedha hizo kupungua ili kukamilisha manunuzi yaliyokuwa yamekusudiwa, pamoja pamoja na baadhi ya vifaa vilivyoelezwa kukosekana MSD. Kamati iliazimia kwamba, Menejimenti kupitia idara ya afya itoe fedha kwa ajili ya kuongezea kiasi kilichopungua ili vifaa ambavyo havijanunuliwa vinunuliwe kule zahanati.

6. **TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 390,000,000/= NA KUWASILISHA MGAWANYO WA FEDHA KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARULA (EMD) NA UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI (3/1) KATIKA KITUO CHA AFYA KIRUMI.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha jumla ya Tshs 390,000,000/= zikiwa na mchanganuo wa kutekeleza miradi ifuatayo.

1. Ujenzi wa jengo moja la wagonjwa wa dharula  katika hospitali ya wilaya ya Butiama kiasi cha Tshs. 300,000,000/=.

2. Ujenzi wa nyumba ya moja ya watumishi (3/1) katika kituo cha Afya Kirumi kiasi cha Tshs 90,000,000/=.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuelekeza utekezaji ufanyike kwa wakati na ubora aidha waliipongeza serikali kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

**KUMB NA KFUM/04/21/2021/2022 TAARIFA YA FEDHA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA MWEZI NOV. 2021**

Taarifa hiyo iliwasilishwa na kupokelewa. Katika kuwasilisha taarifa hiyo Mweka Hazina (W) alisema kuwa, kwa mwaka wa fedha2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Butiama imekasimia kukusanya jjumla ya Tsh. **39,630,822,426.00** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Makisio ya mapato haya yanatokana na vyanzo vifuatavyo-;

- Vyanzo vya ndani vya Halmashauri yenyewe – **1,545,234,388.00**
  **RUZUKU**

- Mishahara PE – Tsh. 30,422,160,288
- Matumizi mengineyo – OC Idara nyingine – 831,891,600.00
- Miradi ya maendeleo – 6,831,536,150.00

  Hivyo kufanya jumla ya mapato – 39,630,822,426.00

Aidha kuhusu mapato, ilielezwa pia kwamba, kwa kipindi cha mwezi Nov. 2021, kiasi cha Tsh. **71,435,486.38** kimekusanywa kutokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri yenyewe. Aidha fedha za Ruzuku zilizopokelewa ni Tsh. **1,671,431,240.80**.
Baada ya mjadala wa kina kamati ilisisitiza menejimenti kukusanya kikamilifu vyanzo vyote ili kuinua mapato. Taarifa ilipokelewa.

**KUMB NA KFUM/04/22/2021/2022 MAPENDEKEZO YA MAHAULISHO(MAREKEBISHO YA BAJETI) YA MWAKA 2021/2022**

Wajumbe walifahamishwa kwamba, mahaulisho hayo yanatokana na sharia ya bajeti ya 2015, na hii ni kutokana na hali ya hewa kuathiri uzalishaji wa mazao hivyo kusababisha kupunguza tozo. Pamoja na kupanda kwa gharama na bei za bidhaa mbalimbali. Kamati ilipokea na kuridhia taarifa hiyo.

**KUMB. NA. KFUM/04/22/2021/2022 TAARIFA YA ZOEZI LA CHANJO YA MIFUGO DHIDI YA UGONJWA WA MAPELE YA NGOZI.**

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa, isipokuwa kamati iliazimia kwamba, Timu ya Menejimenti ipitie kikamilifu Mkataba wa utekelezaji wa zoezi hili kisha Mkataba huo uwasilishwe katika kikao cha Kamati ya Fedha Utawala na Mipango kinachofuata.

**KUMB. NA. KFUMU.08/72/2021/2020 MENGINEYO**

Mhe. Diwani Kata ya Sirorisimba alitoa taarifa ya kuwepo kwa daraja bovu ambalo linasababisha kutopitika hususani katika kipindi cha mvua. Aidha kamati ilipokea taarifa hiyo ambapo iliagiza kwamba Mkurugenzi Mtendaji awasilishe suala hili katika Ofisi ya Mhe Mkuu wa Wilaya.

**KUMB NA KFUM/08/72/2020/2021 KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 07:20 mchana. aliwashukuru wajumbe na wataalam kwa ushiriki wao. Pia alisisitiza juu ya utekelezaji wa maelekezo pamoja na maazimio yaliyotolewa na Kamati.

UMETHIBITISHWA

Jina ..........................  Jina ..........................

Saini ..........................  Saini ..........................

14/01/2022

**TAREHE**